**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

*(Barua zote zipitie kwa mkuu wa Shule ya Sekondari Digodigo)*

*Ofisi ya Mkuu wa Shule*

**MKUU WA SHULE**
*SIMU. No. +255785758063*
*+255754088341*

**S.L.P 23,**
**LOLIONDO.**

**04.12.2019**

MAKAMU MKUU WA SHULE
0786337288
0766153881

**OFISI YA MALEZI**
0753515202
0757058824

Kumb Na:DD/SS/FIJ/VOLI.1/21

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi,

.......................................................................

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KIDATO CHA KWANZA 2020**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao

...........................................................

Amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Digodigo.

**SIKU YA KUFUNGUA SHULE.**

Shule itafunguliwa tarehe 05/01/2020 siku ya jumapili na mwanao anapaswa kuripoti siku hiyo hiyo kuanzia saa 04:00 asubuhi na mwisho wa kuripoti ni saa 09:30 alasiri siku hiyohiyo maana jumapili haitakuwa siku ya kazi na jumatatu masomo yataanza rasmi. Atakayekuja baada ya tarehe 05/01/2019 atakuwa amechelewa.

**A: Sare ya shule na mavazi mengine ya kushindia shuleni**

i. Suruali kama ni mvulana au sketi kama ni msichana mbili (2)za shule rangi ya dark blue . Suruali ziwe na mifuko miwili (2) mbele na moja (1) nyuma pia upana miguuni inchi 18.

ii. T _shirt (2) zenye nembo ya shule. (zinapatikana shuleni kwa Tshs 7,000/= kwa kila moja).

iii. Sweta mbili (2) rangi ya dark blue (zinapatikana kwa Tshs 13,500/=).

iv. Mashati meupe mawili ya mikono mifupi (tomato).

v. Tai ya blue ndefu yenye mistari meupe (pia zinapatikana shuleni kwa Tshs 3,500/= )

vi. Viatu vya ngozi vyeusi na visivyo na visigino virefu jozi mbili vya kufunga na kamba.

vii. Soksi jozi mbili nyeupe kama ni msichana na khaki kama ni mvulana.

viii. Raba na bukta za michezo.

ix. Suruali za kitambaa rangi ya khaki kama ni mvulana na kijani kama ni msichana na blouse yake kwa ajili ya kushindia.

x. Tracksuit ya blue yenye mstari meupe, pia zinapatikana maduka karibu na shule.

NB: Vifaa vyote hapo juu vinapatikana duka iliyopo karibu na shule. Husimcheleweshe mwanao kwa kusubiri kushonewa nguo mtaani. Suruali moja ya dark blue Tshs 18,000/= suruali ya kaki Tshs 17,000/= sketi ya dark blue Tshs 18,000/= shamba dress (suruali na blouse kwa wasichana ni Tshs 32,000/=

**B: vifaa vya masomo**

- ✓ Uje na kounta book 10 (quire 2 or 3), daftari za graph(graph pad )1, madaftari madogo kumi (10) na kalamu za kutosha,Mkebe (mathematical set).
- ✓ Kamusi (oxford) English to English.
- ✓ Begi la kubebea madaftari na vitabu (mifuko ya plastiki ni marufuku).
- ✓ Mnunulie mwanao saa ya mkononi ili aweze kutunza muda.
- ✓ Unaombwa umnunulie mwanao vitabu vya kutosha kama vile;

i. BIOLOGY BOOK ONE (oxford)

ii. Physics book one (oxford)

iii. Mathematics book one (oxford)

iv. Kiswahili kidato cha kwanza (oxford)

v. English book one (oxford)

vi. Civics book one (oxford)

vii. Geography book one (oxford)

viii. History book one (oxford)

ix. Kitabu chochote cha michezo kama utakipata kwani shule hii ni ya michezo.

**C: Vifaa Vingine.**

- Aje na godoro lenye upana wa futi mbili na nusu nchi 4 (magodoro ARUSHA/(TANFOM) au SUPER BANCO) aina nyingine HAZITAPOKELEWA kwani zinadumu kwa mwaka moja tu.
- Sanduku la bati kwa ajili ya kutunza vifaa vyake.
- Aje na vifaa vya usafi kama ufagio wa chelewa, jembe na mpini wake kwa wavulana panga kwa wasichana na ndoo ya kuogea lita kumi.
- Aje na taulo na kanga mbili kwa wasichana.
- Wasichana aje na pedi angalau pakiti nne.
- Aje na vyombo vya kulia kama sahani, kikombe, bakuli na kijiko.
- Aje na sabuni za kutosha dawa ya meno, mswaki na mafuta ya kupaka yasiyo na harufu kali.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula.
- Mpatie mwanao fedha za matumizi (pocket money) angalau 50,000/= au zaidi
- Aje na toilet paper angalau pakti 4.
- Aje na chandarua (net) kwa ajili ya kujikinga na mbu nyeupe kwa wasichana na kijani kwa wavulana.
- Aje na shuka mbili rangi ya blue kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.
- Viatu vya kushindia vya wazi (open shoes) maana yeboyebo haziruhusiwi shuleni.

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebshwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu – TAMISEMI lenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi , wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali ya umma.
- Kutunza mali za umma.
- Ni marufuku mwanafunzi kuongea na mgeni yeyote bila ruhusa ya mwalimu.
- Ni marufuku kwenda kwenye nyumba za watumishi bila ruhusa.
- Kuheshimu bendera.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO.**

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
v. Kupigana na kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
vii. Kudharau bendera ya taifa.
viii. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kutoa mimba
xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa au kujaribu kukataa adhabu kwa makusudi.
xiii. Kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu.

MUHIMU.

a) Atatakiwa apime kuthibitisha afya yake kwenye hosipitali ya serikali. (Fomu imeambatanishwa kwenye barua hii).
b) Shule haitoi chakula maalum kwa waonjwa (special diet)
c) Utapokelewa iwapo umeyatekeleza maagizo yote yaliyotolewa hapo juu.
d) Simu haziruhusiwi hapa shuleni (ukikamatwa na simu utarudishwa nyumbani).
e) Tafadhali soma kwa makini maelekezo au maagizo hayo na kuyatekeleza kwa umakini.

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DIGODIGO.***

…………………………

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI DIGODIGO

Nakala:

Mthibiti ubora kanda
Kanda ya kazkazini magharibi,
SL.P. 807,
Arusha.

Afisa elimu (m) Arusha,
S.L.P. 2032,
Arusha.

Mkurugenze mtendaji,
Halmashauri ya (w)Ngorongoro ,
SL.P. 01,
Arusha.

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

To be completed by the government medical officer.
Pupil's full name ……………………………………………………….
Blood count (red and white)……………………………………………..
Stool examination………………………………………………………………..
Urinalysis…………………………………………………………………
T.B test ……………………………………
Eye test…………………………………
Ear's test…………………………………..
Chest……………………………………
Spleen……………………………………………………………
Girls UPT test…………………………………..
HP test ……………………………………………………………
Additional information e.g. Physical defects or impairment infection chronic or family shape etc.
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………

**TO BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER.**

I certify that the above mentioned pupil is able/unable to pursue his/her further studies.
Signature…………………………..
Designation……………………….
Station …………………………….
Date ………………………………..